## UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa msaada wa Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) ikishirikiana na Taasisi ya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii (ESRF) inatekeleza Mradi wa Kupunguza Umaskini na Kuhifadhi Mazingira.

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali katika Halmashuri za Nyasa, Ikungi, Ileje, Bunda, Bukoba Vijijini na Sengerema pia Jeshi la Kujenga Taifa, Mashirika ya Kiraia, na Vikundi vya wananchi katika Wilaya husika.

## MIRADI YA KILIMO

Kupitia Mradi huu kumekuwepo na utekelezaji wa miradi kadhaa ya kilimo, kwa kushikirikiana na wadau mbalimbali. Ubunifu katika kilimo umemsaidia mkulima kupata mazao mengi na yenye ubora kwa kutumia eneo dogo la ardhi na kwa gharama nafuu. Mradi ulitumia fursa ya kukua kwa teknolojia duniani, hususani katika kilimo (Shamba Kitalu, Azolla, Kilimo bila Udongo nk), kuwezesha wakulima katika Wilaya husika kutumia eneo dogo la ardhi kuzalisha mazao mengi na yaliyo bora.

Matumizi ya Jukwaa la MKilimo (mkilimo.esrf.or.tz) yamewezesha wakulima kupata taarifa mbalimbali zihusuzo kilimo cha kisasa toka kwa wataalam kwa haraka na kwa muda muafaka hivyo kusaidia kupata mavuno mengi na bora. Halikadhalika jukwaa hilo limewasaidia wakulima kupata masoko ya mazao yao kwa urahisi.

KILIMO cha kutegemea teknolojia za kisasa kinatekelezwa na JKT katika Kambi ya Ruvu, iliyopo Wilaya ya Kibaha, ambapo wanazalisha mbogamboga pamoja na chakula cha mifugo. Alikadhalika kilimo hiki kinafanywa na kikundi cha Wakulima Nyatwali katika Wilaya ya Bunda (Kilimo cha mboga mboga, chakula cha mifungo na mbolea) na pia kinafanywa na mkulima bingwa Bw. Ahmed Mbae, wa Kemondo katika wilaya ya Bukoba Vijijini ambaye anatumia kilimo hiki kuzalisha chakula cha mifugo.



*Uzalishaji wa chakula cha mifugo (Hydroponic fodder) – Kemondo – Bukoba Vijijini*

Kilimo cha kutumia technolojia pia kinajumuisha matumizi ya Shamba Kitalu yaani "Green House" Mradi huu umetekelezwa na JKT katika kiteule cha Bulamba na kikundi cha wakulima Nyatwali. Mashamba Kitalu yamesaidia sana kupunguza madhara yanayosababishwa na wadudu waaribifu na hivyo kuongeza uzalishaji na kupatikana kwa mazao yenye thamani kubwa.



*Vijana waliojiunga JKT katika mafunzo ya kuhudumia shamba kitalu. Elimu hii itawasaidia baada ya kukamilisha mafunzo yao.*



*Mazao yaliyotumia Azolla kama mbolea katika kijiji cha Nyatwali*

**"Azolla naitumia zaidi kama mbolea, matokeo yake ni mazuri, mbogamboga na migomba inastawi sana" Hamad Nyamanda – Mwanachama, Kikundi cha wakulima `Nyatwali.**



*Mazao yaliyooteshwa kwenye mfumo wa Kilimo bila udongo pamoja na samaki - Nyatwali*

Kilimo bila kutumia udongo pamoja na ufugaji samaki (Aquaponic) katika kilimo hiki kinyesi cha samaki kinatumika kurutubisha mbogamboga na udongo hautumiki. Ubunifu huu unapatikana Ruvu JKT na Nyatwali katika Wilaya ya Bunda.

Kilimo cha Azolla, ni kilimo cha majani yanayo ota kama magugu maji katika mito na mabwawa, Azolla imegundulika kuwa chakula kizuri sana cha mifugo mbalimbali kama vile samaki, ng'ombe, mbuzi n.k. Pamoja na kuwa chakula bora kwa mifugo, Azolla pia ni mbolea nzuri sana kwa mazao mbalimbali. Azolla imesaidia sana katika kupunguza gharama za chakula cha mifugo, lakini pia mifugo inayotumia Azolla inakua na afya nzuri.



*Mabwawa ya Azolla katika shamba la bw. Ahmed Mbae, Kemondo Bukoba Vijijini*

**"Azolla imenisaidia kupunguza ghalama za chakula cha mifugo yangu kwa asilimia 30%" Bw. Ahmed Mbae – mkulima bingwa Bukoba vijijini.**

## MIRADI YA UFUGAJI WA NYUKI

Kupitia Mradi wa Kupunguza Umaskini, miradi kadhaa ya ufugaji nyuki inatekelezwa katika Wilaya za Ileje, Nyasa na Ikungi. Wanawake na vijana katika Wilaya hizo tatu walijengewa uwezo katika ufugaji wa nyuki, na jinsi ya kutumia



Mizinga ya kisasa ya nyuki

mizinga ya kisasa na vifaa maalumu vya kurinia mazao yatokanayo na nyuki. Kama sehemu ya Mradi vikundi viligawiwa mizinga ya kisasa na zana bora za kuvunia mazao ya nyuki kama vile; asali na nta. Wananchi wengi wameelezea mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kipato na ubora wa asali. Alikadhalika kutokana na Mradi huu wananchi wamepata mwamko wa kutunza mazingira na hivyo kulinda uoto wa asili.

## UFUGAJI WA SAMAKI

Katika kupambana na matatizo ya uvuvi haramu na upungufu wa samaki katika maziwa na mito, Mradi wa Kupunguza Umaskini na Kuhifadhi Mazingira unatekeleza miradi ya ufugaji wa samaki katika Wilaya tatu. Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wameanzisha mradi wa ufugaji wa samaki katika vizimba. Mradi huu wa aina yake hapa Tanzania umesaidia kuongeza uzalishaji wa samaki lakini pia kulinda mazingira ya ziwa Victoria. Wavuvi na wananchi kwa ujumla katika vijiji vinavyozunguuka mradi, wamehamasika na ufugaji na utunzaji wa mazingira. Matumizi ya milipuko, nyavu zisizostahili na sumu katika eneo la mradi yamepungua sana.

Hivi karibuni JKT kwa kushirikiana na ESRF kwa ufadhili wa UNDP wameanza kujengea uwezo vikundi vya wanawake na vijana ili vianzishe ufugaji wa samaki katika vizimba. Ufugaji huu utafanyika katika maeneo yaliyobainishwa katika Wilaya za Bunda na Bukoba Vijijini. Lengo la ufugaji huu ni kusaidia kupata samaki wengi hivyo kuongeza kipato cha wafugaji, na kutunza mazingira ya ziwa Victoria.



*Ufugaji wa kisasa wa samaki kwa kutumia vizimba unaotekelezwa na JKT Rwamkoma katika eneo la Karukekere*

**“Vijana wanaojiunga na JKT kwa hiari au kwa mujibu wa sheria wananufaika sana na mafunzo wanayopata kupitia miradi hii. Ujuzi wanaoupata unawasaidia kujiajili wanapomaliza mafunzo yao” Maj. DJ Msakulo, Mkuu wa Kikosi cha JKT Rwamkoma.**

Mradi wa Kupunguza Umaskini na Kuhifadhi Mazingira pia unatekeleza miradi ya ufugaji wa samaki katika mabwawa. Mradi ulifadhili uchimbaji wa mabwawa makubwa na ujenzi wa kitotoleshi (Hatchery) katika eneo la JKT Bulamba ili kurahisisha upatikananaji wa vifaranga bora kwa bei nafuu. Alikadhalika mabwa manane kwa ajili ya ufugaji wa samaki Sato na Kambale yamechimbwa ili kuzalisha samaki lakini pia kama sehemu ya kutolea mafunzo kwa vijana wanaojiunga na JKT na jamii kwa ujumla.



*Mabwawa ya samaki na kitototoleshi cha samaki (Hatchery) yaliopo katika Kiteule cha JKT Bulamba*



## UFUGAJI WA KUKU

Ni shughuli nyingine ambayo mradi umefadhili ili kumwongezea mwananchi kipato. Mradi wa Kupunguza Umaskini na Kuhifadhi mazingira umekuwa unatoa mafunzo kwa watu mbalimbali juu ya ufugaji wa kuku kisasa. Familia nyingi maskini zimenufaika kutokana na mradi huu.

*Banda la kuku waliofugwa kisasa – Banda la mama Kalega, Bukoba*

## BIOGAS

Mradi pia ulitekeleza mradi wa kuzalisha nishati kwa kutumia kinyesi cha mifugo yaani biogas. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Sengerema, Mkoa wa Mwanza ili kukabiliana na hali ya kupungua kwa kasi kwa Misitu katika Wilaya hiyo. Kaya zilizopatiwa mtambo wa biogas zinaripoti kupunguziwa tatizo la nishati ambayo hapo awali iliwagharimu akina mama muda mrefu kufuatilia kuni toka mbali. Pia magonjwa yaliyosababishwa na moshi yamepungua sana na watoto washule wanaweza kujisomea kutokana na taa zinazowashwa na biogas.

*Kwa kufahamu zaidi miradi hii tembelea* **tinyurl.com/maarifa**

MRADI HUU UNAFADHILIWA NA SHIRIKA LA MAENDELEO LA UMOJA WA MATAIFA (UNDP) NA SHIRIKA LA UMOJA WA MATAIFA LA MAZINGIRA (UNEP). KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA TAASISI YA TAFITI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII (ESRF) 0754 780 133, 0655 780 233. BARUA PEPE esrf@esrf.or.tz, NA JESHI LA KUJENGA TAIFA, BARUA PEPE info@sumajkt.go.tz

**Economic and Social Research Foundation (ESRF)**
51 Uporoto Street, off Ali Hassan Mwinyi Road
P.O. Box 31226, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: (+255-22) 2926084-9 • Fax: (+255-22) 2926083
E-mail: esrf@esrf.or.tz • Website: www.esrftz.org

# MRADI WA KUPUNGUZA UMASKINI NA KUHIFADHI MAZINGIRA

Kujenga uwezo wa wananchi katika kupambana na umaskini na kuhifadhi mazingira kupitia:

- Kilimo bora kinachotumia technolojia ya kisasa (Smart Farming)
- Ufugaji wa Samaki
- Ufugaji wa Nyuki
- Biogas na
- Kujenga uwezo wa wanawake na vijana.

Mradi Huu unatekelezwa kwa ushirikiano wa Halmashauri za Wilaya Sita, Jeshi la Kujenga Taifa Na Vikundi vya Akina Mama Na Vijana. Unasimamiwa na Taasisi ya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii (ESRF) Na Kufadhiliwa Na Shirika la Maendeleo la Umoja Wa Mataifa (UNDP/UNEP) na Serikali ya Tanzania.